NISHATI | HABARI ZA NISHATI
News Bulletin
www.nishati. go.tz Wizara ya Nishati wizara_ya_nishati_tanzania @Nishati2017 Wizara ya Nishati
Toleo Namba 13 Aprili 1-30, **2020**

# SERIKALI IMEJIPANGA KUHAKIKISHA MAFUTA YANAPATIKANA MUDA WOTE



*Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani (aliyesimama) akizungumza na wadau wa mafuta nchini (hawapo pichani) katika kikao kilichofanyika kwenye ofisi za Wakala wa Uagizaji Mafuta Kwa Pamoja (PBPA), jijini Dar es Salaam, Machi 17, 2020. Kushoto ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini Dunstan Kitandula na kulia ni Katibu Mkuu Wizara ya Nishati Mhandisi Zena Said.*

UK. 2

## KAMATI YA BUNGE YAWASHA UMEME KISEMVULE

UK. 4

JARIDA HILI HUTOLEWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI
Wasiliana nasi kwa simu namba +255-26-2322018 Nukushi +255-26-2320148 au Fika Ofisi ya Mawasiliano, Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P. 2494, 40474 Dodoma

# SERIKALI IMEJIPANGA KUHAKIKISHA MAFUTA YANAPATIKANA MUDA WOTE

*Hafsa Omar - Dar es Salaam*



*Kutoka kushoto ni Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani, Katibu Mkuu Wizara ya Nishati Mhandisi Zena Said na Naibu Katibu Mkuu Mhandisi Leonard Masanja wakiwa pamoja na wadau mbalimbali wa mafuta (hawapo pichani) wakijadili hatua ambazo nchi itazichukua endapo uhaba wa mafuta utajitokeza katika kipindi hiki cha Mripuko wa maradhi ya Virusi vya Corona, jijini Dar es Saalam, Machi 17, 2020.*

Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani, amekutana na kufanya mazungumzo na wadau wa mafuta nchini kujadili hatua ambazo nchi itazichukua endapo uhaba wa mafuta utajitokeza katika kipindi hiki cha mlipuko wa maradhi ya virusi vya Corona.

Mkutano huo ulifanyika Machi 17, 2020 jijini Dar es Salaam, katika ofisi za Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) na kuhudhuriwa na Katibu Mkuu Wizara ya Nishati Mhandisi Zena Said, Naibu Katibu Mkuu Mhandisi Leonard Masanja, Kamishna wa Petroli na Gesi Adam Zuberi, viongozi mbalimbali wa Taasisi za Wizara pamoja na wadau wa mafuta nchini.

Akieleza dhumuni la Mkutano huo, Dkt Kalemani alisema kuwa, ni kwa ajili ya kujadiliana ili kuona namna bora ya kuhakikisha mafuta yatapatikana muda wote kulingana na mahitaji ya nchi.

"Sisi kama Serikali pamoja na wadau ni jukumu letu kuhakikisha kwamba mafuta yanapatikana muda wote, tena ya kutosha kuendesha shughuli zenu wafanyabiashara lakini na kuendesha shughuli za Serikali pamoja na shughuli za kijamii," alisema.

Alisema kuwa nchi inajenga miradi mingi mikubwa ya kimaendeleo na kwa kiasi kikubwa miradi hiyo inategemea mafuta katika kuendesha shughuli zake.

Aliongeza kuwa, nchi ambazo Tanzania inanunua mafuta, mpaka sasa bado wanaendelea na uzalishaji wa mafuta na bado hawajafunga mipaka yao, lakini kwa upande wa serikali lazima ichukue hatua madhubuti kwa kushirikiana na wadau wake ili kuweza kujipatia mafuta ya kutosha nchini.

Hata hivyo, Dkt Kalemani amewatoa wasiwasi watanzania kwamba mafuta yapo ya kutosha na kwamba akiba iliyopo inaweza kutosheleza mahitaji ya nchi kwa kipindi cha miezi miwili ijayo.

Alisema, japokuwa nchi ina mafuta ya kutosha kwa kipindi hiki lakini ni lazima itafute kinga badala ya kusubiri kuhangaika na tiba.

Kwa upande wao, wadau wa mafuta nchini, waliipongeza Serikali kwa kitendo cha kuwaita ili kuzungumzia suala husika na kuahidi kuwa wapo tayari kutoa ushirikiano ili kuhakikisha mafuta yanapatikana nchini muda wote.

Aidha, walitoa ushauri wa njia mbalimbali ambazo wanaona zikichukuliwa zitasaidia katika kukabiliana na uhaba wa mafuta endapo changamoto hiyo itajitokeza siku zijazo.

Njia hizo ni pamoja na kutafuta wazalishaji wa mafuta wa nchi nyingine endapo wale wazalishaji wa awali watafunga mipaka ya nchi zao katika kipindi hiki cha mpito.



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati Mhandisi Zena Said (aliyesimama), akizungumza kwenye kikao baina ya Waziri wa Nishati na wadau mbalimbali wa Mafuta nchini, jijini Dar es Salaam, Machi 17, 2020. Kushoto ni Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani na kulia ni Naibu Katibu Mkuu, Mhandisi Leonard Masanja.*



*Wadau mbalimbali wa mafuta nchini wakiwa katika kikao cha pamoja baina yao na Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (hayupo pichani), kilichofanyika Machi 17, 2020 ofisi za Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) jijini Dar es Salaam.*

# EWE MDAU WA NISHATI CHUKUA TAHADHARI DHIDI YA CORONA

Kwenu wasomaji na wadau wetu wa sekta ya nishati. Leo, tunawiwa kuzungumzia janga hili la kimataifa la ugonjwa wa Corona (COVID-19) ambalo linaendelea kuitesa Dunia.

Kupitia jukwaa hili, tunawakumbusha na kuwasisitiza kufuata maelekezo yote yanayoendelea kutolewa na viongozi wetu wakuu wa serikali pamoja na wataalamu wa afya katika kujikinga na janga hili.

Tumewiwa kusisitiza hili kutokana na utafiti usio rasmi, ambao unaonesha kuwa wako baadhi ya wananchi ambao bado wanapuuza ama hawalichukulii kwa uzito unaostahili janga hili hivyo hawatekelezi ipasavyo maelekezo yanayotolewa na mamlaka husika.

Kuna msemo maarufu wa wahenga usemao “Asiye sikia la mkuu huvunjika guu” na mzaha mzaha hutumbuka usaha!!” Ugonjwa wa COVID -19 upo na kamwe tusichukulie mzaha!! Tunayo mifano ya nchi kama Italia na Uhispania ambazo wakati ugonjwa huu umeingia katika nchi ya China, hawakulichukulia janga hilo kwa uzito unaostahili na matokeo yake sasa nchi hizo ni miongoni mwa zinazoongoza kwa maambukizi.

Tunapenda kuwaarifu kwamba Wizara ya Nishati inalichukulia kwa uzito wa hali ya juu janga hili na tayari inatekeleza maelekezo yote yaliyotolewa na viongozi wakuu wa serikali pamoja na wataalamu wa afya.

Aidha, katika kuhakikisha Taasisi zilizo chini ya Wizara pia zinatekeleza maagizo hayo ipasavyo, viongozi wa Wizara wamekuwa wakitembelea na kufanya ukaguzi katika ofisi mbalimbali za Taasisi.

Hivi karibuni Naibu Waziri wa Nishati Subira Mgalu alitembelea Ofisi za Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Mkoa wa Morogoro na kupongeza hatua ambazo shirika hilo limekuwa likichukua katika kuhakikisha linawakinga watumishi na wateja wake dhidi ya ugonjwa huo kadri ya uwezo wake.

Jitihada hizi zote zinazofanywa na Wizara hazitakuwa na maana na hazitazaa matunda pasipo ninyi wadau wetu kutoa ushirikiano. Hivyo basi, tunategemea kuanzia sasa, kwa wale ambao walikuwa hawalichukulii suala hili kwa uzito, wataanza kufanya hivyo.

Hata hivyo, kama ambavyo Mheshimiwa Rais wetu John Pombe Magufuli ametuasa pia, pamoja na kuchukua tahadhari kadri tunavyoelekezwa lakini pia tusisahau kumwomba Mungu, kila mmoja kwa imani yake ili atuepushe na janga hili.

Sote tukitimiza wajibu wetu pamoja na kumwomba Mungu, bila shaka atatuepusha na janga la CORONA.

# Katunika Ki-nishati







## BODI YA UHARIRI

**Mhariri**
**Veronica Simba**
(Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini)

**Waandishi**
**Veronica Simba**
**Teresia Mhagama**
**Zuena Msuya**
**Hafsa Omar**

**Msanifu Kurasa**
**Lucas Gordon**

Wasiliana nasi kwa simu namba +255-26-2322018
Nukushi: +255-26-2320148
au

Fika Ofisi ya Mawasiliano Mtumba Dodoma, S.L.P. 2494, 40474 Dodoma

*www.nishati. go.tz*
*Wizara ya Nishati*
*@Nishati2017*
*wizara_ya_nishati_tanzania*
*Wizara ya Nishati*

# KAMATI YA BUNGE YAWASHA UMEME KISEMVULE



*Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Vedastus Mathayo (mwenye mkasi), akikata utepe kabla ya kuwasha rasmi umeme katika Zahanati ya Kijiji cha Kisemvule, wilayani Mkuranga, Mkoa wa Pwani, Machi 17, 2020. Kushoto kwake ni Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu.*



*Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Vedastus Mathayo, akibofya king'ora maalum kuashiria kuwasha rasmi umeme katika Zahanati ya Kijiji cha Kisemvule, wilayani Mkuranga, Mkoa wa Pwani, Machi 17, 2020. Kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga Filberto Sanga na mwenye ushungi ni Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu.*

**Veronica Simba – Pwani**

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini imewasha umeme katika Zahanati ya Kijiji cha Kisemvule, kilichopo Mkuranga, Mkoa wa Pwani.

Tukio hilo lilifanyika Machi 17 mwaka huu, wakati Kamati hiyo ikiwa katika ziara kukagua miradi ya umeme vijijini mkoani Pwani.

Akizungumza katika hafla hiyo, Kaimu Mwenyekiti wa Kamati, Vedastus Mathayo, aliwahamasisha wananchi kuchangamkia fursa ya uwepo wa Mradi wa Umeme Vijijini (REA) katika eneo hilo kutokana na gharama yake nafuu ya shilingi 27,000 tu.

"Serikali ya Awamu ya Tano imeamua kuwaletea umeme huu wa gharama nafuu. Changamkieni fursa, mlipie kwa wingi ili kila mmoja aunganishiwe huduma hii kwa ajili ya kujiletea maendeleo."

Awali, akitoa taarifa ya utekelezaji wa miradi ya umeme katika Wilaya ya Mkuranga kwa Kamati, Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, alisema mpaka sasa vijiji 44 kati ya 125 vimekwishapelekewa umeme kupitia Mradi wa Umeme Vijijini, Awamu ya Tatu, Mzunguko wa kwanza.

Alieleza zaidi kuwa, kwa kutambua umuhimu wa nishati ya umeme kwa wananchi na kwa namna Wilaya hiyo inavyokua kwa kasi, Serikali iliamua kuongeza wigo wa Mradi ili kuwafikia wananchi wengi zaidi na kwamba kazi inaendelea.

"Katika wigo wa awali, Mkandarasi alikuwa ameshaunganisha wateja 6,000. Mahitaji yakawa makubwa, Serikali ikaongeza wateja wapya takribani 4,000 na kazi inaendelea," alieleza Naibu Waziri.

Alisema kuwa, matarajio ya Serikali hadi ifikapo Juni mwakani, maeneo yote yawe yamefikiwa na umeme kwa kiasi kikubwa.

Kwa mujibu wa taarifa ya Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mradi wa REA Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Kwanza mkoani Pwani utanufaisha vijiji 150 ambapo mpaka sasa vijiji 115 tayari vimekwishawashiwa umeme.

Aidha, mbali na mradi wau meme vijijini, iko miradi mingine ya umeme inayoendelea kutekelezwa mkoani humo ikihusisha Peri-Urban, Ujazilizi (Densification) na miradi mingine inayotekelezwa na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).



*Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, Filberto Sanga akitoa salamu za ukaribisho kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, ilipotembelea Kijiji cha Kisemvule na kuwasha umeme katika Zahanati yake, Machi 17, 2020.*



*Naibu Waziri wa Nishati Subira Mgalu, akitoa salamu za ukaribisho kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, ilipotembelea Kijiji cha Kisemvule na kuwasha umeme katika Zahanati yake, Machi 17, 2020. Kulia ni Kaimu Mwenyekiti wa Kamati, Vedastus Mathayo na kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, Filberto Sanga.*




*Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Ally Kessy akiwa mbele ya Zahanati ya kijiji cha Kisemvule, wilayani Mkuranga, Mkoa wa Pwani. Kamati husika iliwasha rasmi umeme katika Zahanati hiyo, Machi 17 mwaka huu wakiwa katika ziara ya kazi kukagua miradi ya umeme vijijini.*

# KAMATI YA BUNGE YAWASHA UMEME KISEMVULE





*Baadhi ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, wakiwa katika hafla ya uwashaji umeme katika Zahanati ya Kijiji cha Kisemvule, Mkuranga, mkoani Pwani, Machi 17 mwaka huu.*





*Sehemu ya umati wa wananchi wa kijiji cha Kisemvule, wilayani Mkuranga, Mkoa wa Pwani, wakifuatilia hafla ya uwashaji rasmi umeme katika Zahanati ya kijiji hicho, uliofanywa na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini (hawapo pichani), Machi 17 mwaka huu.*




*Sehemu ya umati wa wananchi wa Kijiji cha Kisemvule, wilayani Mkuranga, Mkoa wa Pwani wakitawanyika baada ya kushuhudia uwashaji rasmi umeme katika Zahanati ya Kijiji hicho, uliofanywa na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Machi 17 mwaka huu.*



*Afisa wa Bunge kutoka Wizara ya Nishati, Alex Nduye (kushoto) na Katibu wa Naibu Waziri wa Nishati, Mhandisi Ngereja Mgejwa, wakijadiliana jambo wakati wa hafla ya uwashaji umeme katika Zahanati ya Kijiji cha Kisemvule, wilayani Mkuranga, Mkoa wa Pwani, uliofanywa na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini (hawapo pichani), Machi 17 mwaka huu.*



*Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani akipewa maelezo ya namna ukarabati unavyoendelea kufanyika katika kingo za mto Kilombero baada ya kuathiriwa na maji kutokana na mvua kubwa zinazoendelea kunyesha nchini.*

# Mitambo ya kufua umeme ipo salama – Dkt Kalemani

***Zuena Msuya - Morogoro***

Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani amesema mabwawa ya kufua umeme wa maji nchini yapo salama licha ya kuwa na ujazo mkubwa wa maji kupita kiwango chake kutokana na mito kutiririsha maji mengi ya mvua zinazoendelea kunyesha nchini katika mabwawa hayo.

Hali hiyo imewalazimu wataalamu na wasimamizi wa mabwawa hayo kufungua milango inayozuia maji, ili kuruhusu maji hayo yatoke kwa ajili ya usalama na kuepusha madhara kwa mitambo ya kufua na kuzalisha umeme, mabwawa yenyewe pamoja na jamii zinazozunguka maeneo hayo.

Dkt. Kalemani alisema hayo Machi 20, 2020, baada ya kufanya ziara ya kutembelea Bwawa la Kidatu lililopo wilayani Kilombero mkoani Morogoro na Mtera lililopo wilayani Iringa mkoa wa Iringa, kuona hali ya usalama, uzalishaji wa umeme katika mitambo pamoja na baadhi ya miundombinu ya kusafirisha umeme iliyopata hitilafu kufuatia mvua kubwa zinazoendelea kunyesha.

Katika ziara hiyo alishuhudia zoezi la kufungulia maji kutoka katika mabwawa hayo kwa lengo la kuepusha hatari ya kuvunjika kwa kingo na madaraja ya kuzuia maji, kwa kuwa mabwawa hayo yamejaa maji kupita kiwango chake na bado maji yanaendelea kuingia na kujaa kutoka katika vyanzo mbalimbali vya mito inayotiririsha maji yake katika mabwawa.

Baada ya kuona hali halisi, Dkt Kalemani aliliagiza Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), kushirikiana na Wakala wa Barabara Nchini (TANDROADS) na Taasisi mbalimbali zenye kutumia vifaa vya kudhibiti maji yenye nguvu kubwa kudhibiti maji hayo yasiweze kuleta madhara na athari zozote katika miradi ya kufua umeme wa maji ukiwemo ule wa Mwalimu Nyerere na jamii inayozunguka maeneo husika.

"Hatuwezi kuzuia maji ya mito kutitirika katika mabwawa yetu, lakini tuna uwezo wa kuyazuia yale yaliyofunguliwa yasilete madhara katika miradi ya kuzalisha umeme wa maji ukiwemo ule unaoendelea kujengwa wa Mwalimu Nyerere, kwa kuwa maji yote haya yanakwenda kule. Pia katika jamii na miundombinu yetu. Maji haya ni mengi na yana nguvu kubwa. TANESCO, TANROADS na Taasisi mbalimbali shirikianeni kudhibiti maji haya. Tumieni vifaa vyenye uwezo mkubwa," alisema Dkt. Kalemani.

Akizungumzia ujazo wa maji katika bwawa la Kidatu, Dkt Kalemani alisema kwa hali ya kawaida bwawa hilo lina mita za ujazo 450, lakini Machi 18, 2020 lilifikia mita za

ENDELEA UK. 7



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (kushoto) akipita katika daraja la mto Kilombero huku akishuhudia maji yaliyofurika na kupita kwa kasi kubwa.*



*Maji yakitoka kwa kasi katika Milango mitatu ya bwawa la Kidatu iliyofunguliwa kupunguza wingi wa ujazo wa maji katika bwawa hilo.*

# Mitambo ya kufua umeme ipo salama – Dkt Kalemani



*Maji yakitoka kwa kasi katika Milango mitatu ya bwawa la Mtera iliyofunguliwa kupunguza wingi wa ujazo wa maji katika bwawa hilo lililojaa kupita kiasi kinachotakiwa.*

ujazo 451.5, maji yalijaa hadi mwisho wa bwawa hilo na kuathiri uzalishaji wa umeme katika mitambo yake, hali iliyosababisha baadhi ya Mikoa inayotumia umeme kutoka kituo hicho kukosa umeme ikiwemo Dodoma, Iringa na Mwanza, lakini Machi 20, 2020 yalipungua na kufika 449.

Kuhusu bwawa la Mtera, Dkt Kalemani alisema kuwa kima cha juu kabisa cha ujazo wa maji kutoka usawa wa bahari ni mita za ujazo 498.50, lakini Machi 18, 2020 ilifikia mita za ujazo 498.70 ambayo imezidi kile kiwango kinachotakiwa na linaelekea kufikia mita za ujazo 499 kitu ambacho ni hatari kwa bwawa na taifa kwa jumla kwa kuwa likipasuka litaleta madhara makubwa na kutumia gharama kubwa na muda mrefu kulijenga tena.

"Natoa wito kwa wataalam wetu waendelee kufungulia maji kwa utaratibu ili yasiathiri yanapokwenda na katika bwawa letu, milango yote mitatu mikubwa ya kutolea maji imefunguliwa na maji yanatoka. Wananchi mtuunge mkono kwenye hili na mlikubali kwa faida yetu sote," alisisitiza Dkt. Kalemani.

Sambamba na hilo amewataka wataalamu kufanya doria ya kukagua nguzo zaidi ya 40 zinazosafirisha umeme mkubwa ambazo ziko katika ukanda wa Mto Ruaha Mkuu zilizopata hitilafu baada ya mto huo kufurika maji ili kubaini tatizo lilipo na kulitatua haraka.

"Tuwaombe wenzetu wa Ulinzi na Usalama tuazimane vyombo vya usafiri kama ni ndege za kawaida au helikopta ili wataalamu wetu waweze kufanya doria katika nguzo hizo ambazo zipo umbali wa kilometa 24, waweze kubaini hitilafu hiyo na kuitatua kwa haraka katika maeneo ambayo hayafifiki kwa magari kutokana na mto kujaa maji."

Alisema kuwa kwa sasa kuna makundi mawili ya doria, moja linatoka Morogoro kwenda Kidatu na lingine kutoka Kidatu kwenda Iringa kilipo chanzo cha tatizo la kuharibika njia ya kusafirisha umeme.

Vilevile aliiagiza TANESCO kuhakisha kuwa inakuwa na Boti za kisasa zinazofanya doria katika kila mabwawa, ambapo tayari Mtera wana boti moja na nyingine ipo katika mpango wa manunuzi ambapo ameagiza kuharakishwa kwa mpango huo na kuukamilisha.

Kuhusu miundombinu ya umeme, Dkt Kalemani alisema kuwa serikali imetenga fedha shilingi bilioni 2.5 kwa kila Mkoa kurekebisha na kuboresha miundombinu ya umeme ikiwa ni pamoja na mitambo, nyaya, mashine umba (transfoma) na vipuri vingine.

Aliwataka Mameneja wa TANESCO Mkoa, Wilaya na Kanda kuacha kisingizio cha kuharibika kwa mitambo ili kutoa mgao wa umeme kwa wananchi na kuongeza kuwa ametembelea mitambo hiyo na kujiridhisha kuwa yote ipo salama na maji yamedhibitiwa hivyo ni marufuku wananchi kukosa umeme kwasababu ya miundombinu kwani umeme upo mwingi.

Vilevile alitoa muda wa mwezi mmoja kwa uongozi wa kituo cha kupoza na kusambaza umeme cha Kidatu kuhakikisha mkandarasi aliyepewa zabuni ya kubadilisha Transfoma iliyoharibika tangu mwaka 2018, katika kituo hicho anafanya hivyo kwa mujibu wa makubaliano.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Richard Kasesera ambaye aliambatana na Dkt Kalemani katika bwawa la kufua umeme la Mtera, aliwataka wananchi waliovamia maeneo ya mito na mabonde na kuweka makazi yao, kuondoka maeneo hayo kwa kuwa siyo salama kutokana na mvua kubwa zinazoendelea kunyesha nchini na kusababisha mafuriko.

Vilevile alimhakikishia Waziri kuwa, viongozi wa Mikoa, Wilaya na Serikali za Mitaa wataendelea kushirikiana na Wizara ya Nishati kuhakikisha kuwa mitambo ya kuzalisha umeme inalindwa na kuwa salama wakati wote.

Pia, aliahidi kuwa viongozi hao watatoa ushirikiano katika kudhibiti mafuriko ili yasiathiri uzalishaji wa mitambo hiyo, pamoja na kuunganisha nguvu za kuthibiti maji yanayofunguliwa katika mabwawa ya kuzalisha umeme yasiweze kuathiri jamii na miundombinu kwa ujumla.



*Mwonekana wa bwawa la Kidatu lililojaa maji kupita kiasi kinachotakiwa. Maji hayo yanatoka katika mito inayotiririsha maji mengi ya mvua zinazoendelea kunyesha nchini.*

# MATUKIO PICHANI





*Moja ya nguzo za kusafirisha umeme mkubwa zikiwa ndani ya mto wa Ruaha Mkuu. Awali nguzo hizo zilikuwa mbali na mto huo, lakini kutokana na hali ya mvua nchini mto huo umejaa maji kupita kawaida yake na kuathiri baadhi ya miundombinu.*



*Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani (kulia) na Mkuu wa Wilaya ya Iringa Richard Kasesera (kushoto) wakipata maelezo kutoka kwa Msimamizi wa kituo cha kufua umeme Mtera walipotembelea bwawa na daraja la kituo hicho.*



*Mmoja wa wafanyakazi wa kituo cha kufua umeme wa maji cha Kidatu akisafisha vipuri vya mashine ya kufua umeme iliyopata hitilafu kutokana na kuzidiwa maji.*



*Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani (kushoto), Mkurugenzi Mkuu wa TANESCO, Dkt. Tito Mwinuka (katikati) na Kamishna Msaidizi wa Umeme Wizara ya Nishati, Mhandisi Innocent Luoga (kulia) wakitazama Mtumbwi unaotumiwa na askari wa TANESCO anayelinda na kufanya doria katika eneo la bwawa la Kidatu eneo la Iyovu.*



*Nyumba ya mlinzi wa TANESCO anayefanya doria katika bwawa la Kidatu katika eneo la Iyovu ikiwa imezingirwa na maji baada ya mto Ruaha Mkuu kufurika maji kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha nchini.*



*Mashineumba (transfoma) katika kituo cha kupoza na kusambaza umeme cha Kidatu iliyoharibika tangu 2018 ikiwa kituoni hapo ambapo Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani ametoa mwezi mmoja kwa mtu aliyepewa zabuni ya kubadilisha mashine umba hiyo kufanya hivyo.*

# KAMATI YA BUNGE YATAKA SEKTA BINAFSI ISHIRIKISHWE KUSAMBAZA GESI ASILIA



*Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Dunstan Kitandula (katikati), akizungumza wakati wa majumuisho baada ya Wajumbe wa Kamati hiyo kutembelea baadhi ya makazi yaliyounganishiwa gesi asilia kwa matumizi ya kupikia jijini Dar es Salaam, Machi 14 mwaka huu.*

***Veronica Simba – Dar es Salaam***

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini imeishauri Serikali kushirikisha sekta binafsi katika usambazaji wa gesi asilia nchini ili kuongeza kasi yake, hivyo kuinufaisha jamii ipasavyo.

Hayo yalibainishwa Machi 14, 2020 na Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Dunstan Kitandula wakati akifanya majumuisho baada ya Wajumbe wa Kamati husika kutembelea baadhi ya makazi ya wananchi wa Dar es Salaam, waliounganishiwa gesi asilia kwa matumizi ya kupikia.

Alisema kuwa imani, matarajio na matumaini ya Wabunge ni kuona kasi ya upelekaji wa gesi asilia kwa matumizi ya wananchi, inaongezeka.

"Angalieni mbinu zitakazosaidia kuishirikisha sekta binafsi kwenye usambazaji wa gesi asilia ili twende kwa haraka zaidi."

Aidha, Kitandula aliitaka Wizara ya Nishati na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), kuwasiliana na Mamlaka zinazohusika na Mipango-Miji ili kuweka mkakati wa pamoja utakaohakikisha miji inapangwa kwa namna ambayo itawezesha miundombinu ya gesi asilia kufikishwa katika makazi ya watu na biashara kwa urahisi.

Akitoa mrejesho wa Serikali kuhusu ushirikishwaji sekta binafsi katika usambazaji gesi asilia, Kamishna wa Petroli na Gesi, Adam Zuberi aliiambia Kamati kuwa suala hilo linafanyiwa kazi na tayari upo Mpango - Hamasishi wa usambazaji gesi hiyo nchini.

"Tunafanya kazi hiyo kwa kushirikiana na wenzetu wa Shirika la Maendeleo la Japani (JICA) na tuko katika hatua nzuri," alieleza Kamishna.

Akifafanua zaidi alisema kuwa, lengo la Mpango huo ni uwezekano wa kutumia teknolojia nafuu ya kusambaza gesi asilia nchini ikiwa ni sehemu ya mkakati wa kutekeleza Mpango Kabambe wa matumizi ya gesi asilia nchini.

Zuberi alieleza malengo mengine ya baadaye kwa Mpango husika ni kuwa na mitambo midogo ya kusindika na kuchenjua gesi asilia itakayowezesha kuisafirisha kwa njia mbalimbali yakiwemo magari, badala ya kutegemea usambazaji kwa njia ya bomba peke yake.

Katika hatua za awali za utekelezaji, alisema kuwa Oktoba mwaka jana, Serikali ilipeleka timu ya wataalamu Japani kujifunza namna nchi hiyo ilivyofanikiwa katika usafirishaji gesi na kwamba Februari mwaka huu, kilifanyika kikao cha wadau jijini Dar es Salaam kueleza hatua ya utekelezaji iliyofikiwa katika Mpango huo.

Awali, akiwasilisha taarifa ya usambazaji gesi asilia nchini kwa Kamati, Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, Dkt James Mataragio alisema ili kuongeza kasi ya usambazaji, Serikali imepanga kuendeleza miundombinu ya usafirishaji wake kwa kushirikisha kampuni binafsi katika kujenga miundombinu ya kujaza gesi katika magari pamoja na kuendeleza biashara hiyo.

Alisema kuwa, katika kutekeleza hilo, Julai 2019, TPDC ilitoa tangazo la fursa kwa kampuni binafsi kuweza kuuza gesi kwa rejareja kwa watumiaji wa nishati hiyo katika magari nchini kama ilivyo katika vituo vya mafuta.

"Kampuni 24 zimeonesha nia ya uwekezaji katika biashara ya rejareja ya ujazaji gesi kwenye magari. Kwa sasa, taratibu za kutoa leseni na vibali kwa kampuni hizo zinaendelea," alisema.

Katika taarifa yake, Dkt Mataragio alieleza kuwa hadi kufikia Februari 2020, TPDC imejenga miundombinu wezeshi yenye urefu wa kilomita 10.8 yenye uwezo wa kuunganisha nyumba zaidi ya 10,000.

Aidha, alieleza kuwa, hadi kufikia Februari mwaka huu, jumla ya nyumba 385 na migahawa minne ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) zimeunganishiwa gesi asilia huku lengo likiwa ni kufikia nyumba za awali zipatazo 1,385 jijini Dar es Salaam ifikapo Juni, 2021.

Miradi hiyo ya kusambaza gesi asilia kwa sasa inatekelezwa katika maeneo ambayo tayari kuna miundombinu wezeshi yakihusisha mikoa ya Pwani na Dar es Salaam.



*Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Dunstan Kitandula (katikati) na baadhi ya Wajumbe wa Kamati hiyo, wakizungumza na mmoja wa wakazi waliounganishiwa mtandao wa gesi asilia kwa matumizi ya kupikia (kulia), maeneo ya Mwenge Mlalakua, jijini Dar es Salaam, Machi 14, 2020.*

# KAMATI YA BUNGE YATAKA SEKTA BINAFSI ISHIRIKISHWE KUSAMBAZA GESI ASILIA



*Kutoka kushoto ni Kamishna wa Petroli na Gesi, Adam Zuberi, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Dunstan Kitandula na Kaimu Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Mhandisi Edward Ishengoma, wakiwa wameongozana na Wajumbe wa Kamati husika, kutembelea baadhi ya makazi yaliyounganishiwa mtandao wa gesi asilia kwa matumizi ya kupikia jijini Dar es Salaam, Machi 14, 2020.*



*Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Dkt James Mataragio akizungumza, wakati wa majumuisho baada ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kutembelea baadhi ya makazi yaliyounganishiwa mtandao wa gesi asilia kwa matumizi ya kupikia jijini Dar es Salaam, Machi 14, 2020.*



*Kamishna wa Petroli na Gesi, Adam Zuberi akizungumza wakati wa majumuisho baada ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kutembelea baadhi ya makazi yaliyounganishiwa mtandao wa gesi asilia kwa matumizi ya kupikia jijini Dar es Salaam, Machi 14, 2020.*



*Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini wakiwasili katika moja ya nyumba zilizounganishiwa mtandao wa gesi asilia kwa matumizi ya kupikia, eneo la Mwenge Mlalakua jijini Dar es Salaam, Machi 14 mwaka huu ili kujionea utendaji kazi wake.*

# VIJIJI VILIVYOSAMBAZIWA UMEME NCHINI VYAFIKA ELFU 9



Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani akisalimiana na wananchi mbalimbali wa kijiji cha Buhungu, Kata ya Kigongo, Wilaya ya Chato, mkoani Geita, akiwa katika ziara ya kazi kukagua miradi ya usambazaji umeme vijijini, Machi 13 mwaka huu.



*Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani akicheza na baadhi ya wananchi wa kijiji cha Buhungu, Kata ya Kigongo, Wilaya ya Chato, mkoani Geita, wakati wa ziara yake kukagua miradi ya usambazaji umeme vijijini, Machi 13 mwaka huu.*

***Hafsa Omar - Geita***

Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani, amesema kazi ya usambazaji umeme vijijini nchini inaendelea kwa kasi ambapo mpaka sasa takribani vijiji 9,009 tayari vimeunganishiwa nishati hiyo.

Aliyasema hayo Machi 13, 2020 wakati akizungumza na waandishi wa habari mara baada ya kuwasha umeme katika kijiji cha Buhungu, Kata ya Kigongo, Wilayani Chato, mkoani Geita.

Alisema kuwa, Serikali itahakikisha inapeleka umeme katika vijiji vyote 12,268 vilivyopo nchini katika muda uliopangwa na haitaruka kijiji hata kimoja.

"Kwa sasa kuna Wilaya 35 ambazo vijiji vyake vyote vina umeme na tutafanya hivyo katika wilaya zote za nchi yetu. Ndani ya miaka hii miwili, ni matarajio yetu kuwa itafika mahala katika wilaya zote hakutakuwa na kijiji ambacho kitakuwa hakijafikiwa na umeme," alisema.

Akielezea baadhi ya manufaa ya usambazaji umeme vijijini, alisema ni pamoja na nguvu kazi ya vijana ambao watabaki vijijini kufanya shughuli za kiuchumi na kwamba wananchi watapata huduma bora zinazotokana na umeme katika sehemu zinazotoa huduma za kijamii kama visima vya maji, vituo vya afya, shule na nyinginezo.

"Vijiji kwa sasa vimeshakuwa na sehemu maalumu ambazo watu wanafanya shughuli za kiuchumi hivyo miji nayo inahamia vijijini. Lakini manufaa makubwa ni nguvu kazi ya vijana kwa sasa kubaki vijijini na kufanya shughuli za maendeleo," alisema Dkt Kalemani

Aliongeza kuwa, manufaa mengine makubwa ya uwepo wa umeme ni kuongezeka kwa viwanda nchini ikiwemo katika maeneo ya vijijini, ambapo takwimu zinaonesha kuwa kuna zaidi ya viwanda 55,000 vinavyotokana na jitihada za serikali za kusambaza umeme vijijini na kwenye miji.



*Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani akisaini kitabu cha wageni mara baada ya kuwasili katika kijiji cha Buhungu, Kata ya Kigongo, Wilaya ya Chato, mkoani Geita, akiwa kwenye ziara ya kazi kukagua miradi ya umeme vijijini, Machi 13 mwaka huu.*

# VIJIJI VILIVYOSAMBAZIWA UMEME NCHINI VYAFIKA ELFU 9



*Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Buhungu, Kata ya Kigongo, Wilaya ya Chato, mkoani Geita, akiwa kwenye ziara ya kazi kukagua miradi ya umeme vijijini, Machi 13 mwaka huu.*



*Wananchi wa kijiji cha Buhungu, Kata ya Kigongo, Wilaya ya Chato, mkoani Geita, wakimsikiliza Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani (hayupo pichani). Waziri alikuwa kwenye ziara ya kazi kukagua miradi ya umeme vijijini, Machi 13 mwaka huu.*



*Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani akikata utepe kuashiria kuwashwa kwa umeme katika Kijiji cha Buhungu, Kata ya Kigongo, Wilaya ya Chato, Mkoa wa Geita akiwa kwenye ziara ya kazi kukagua miradi ya usambazaji umeme vijijini, Machi 13 mwaka huu.*

# Dkt Kalemani awapiga Marufuku wakandarasi kulaza nguzo chini



*Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani (kushoto) akisalimiana kwa mtindo wa kugonganisha miguu na mmoja wa wakazi wa kijiji cha Farkwa wilayani Chemba alipofika katika kijiji hicho kuwasha umeme na kukagua maendeleo ya usambazaji wa umeme katika wilaya hiyo hivi karibuni.*

***Zuena Msuya - Dodoma***

Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani ametoa onyo na kupiga marufuku wakandarasi wanaotekeleza Mradi wa Usambazaji Umeme Vijijini (REA) nchi nzima, kulaza nguzo za umeme chini kwa muda mrefu, badala yake ndani ya siku tatu nguzo hizo ziwe zimefikishwa eneo la mradi na kusimikwa.

Pia, ametoa muda wa siku tatu kwa mkandarasi anayetekeleza mradi wa REA mkoani Dodoma kuondoa nguzo zote ambazo zimelazwa chini katika Mkoa huo na kuzisimika katika maeneo husika, kinyume cha hapo Mhandisi anayesimamia mradi husika pamoja na mkandarasi watachukuliwa hatua.

Dkt. Kalemani alitoa onyo hilo Machi 4, 2020, wakati akiwasha umeme katika kijiji cha Farkwa kilichopo wilayani Chemba mkoani Dodoma.

Alisema kumekuwa na tabia ya wakandarasi kuacha nguzo zikiwa chini kwa muda mrefu bila kusimikwa jambo ambalo limesababisha baadhi ya nguzo kuharibika na fedha za serikali kupotea.

Aidha, Dkt. Kalemani aliwataka Wakurugenzi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Mkurugenzi wa REA kuhakikisha wanasimamia maagizo hayo kwa ukaribu na umakini.

"Hili ni onyo la mwisho. Nimepita barabarani nimekuta nguzo zimelala, sasa Meneja wa TANESCO Kanda na Mikoa simamieni maelekezo haya nguzo zote zilizolazwa chini kwenye mikoa yote nchi nzima ziondolewe na zikajengwe," alisema Dkt. Kalemani.

Katika hatua nyingine, Waziri alisema serikali imetoa shilingi bilioni 40.2 kwa ajili ya kupeleka umeme vijijini.

Dkt. Kalemani alisema kuwa Serikali ina vipaumbele vingi vya kuwahudumia wananchi katika sekta mbalimbali ikiwemo ya maji, afya, barabara na elimu lakini bado imetoa fedha nyingi kwa ajili ya kuhakikisha vijiji vyote vinapatiwa umeme.

Alisema pamoja na juhudi za serikali za kupeleka umeme maeneo mengi, lakini bado kuna changamoto kwa baadhi ya maeneo ambayo hayajafikiwa na kuwa serikali inafanya kila liwezekanalo kuiangaza Tanzania yote.

"Na hili ni onyo kwa wakandarasi wote nchi nzima, ni marufuku kuanzia sasa

ENDELEA UK. 14



*Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani (kushoto) na Mkuu wa Wilaya ya Chemba, Saimon Odunga (katikati), wakiteta jambo wakati Dkt. Kalemani alipofika katika Wilaya hiyo hivi karibuni kukagua maendeleo ya usambazaji wa umeme.*



*Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani (kushoto) akitoa maelekezo kwa Mameneja wa TANESCO na REA kusimamia uondoaji wa nguzo za umeme zilizolazwa chini katika baadhi ya vijiji vya Wilaya ya Chemba.*

# Dkt Kalemani awapiga Marufuku wakandarasi kulaza nguzo chini



*Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani (kushoto) akikagua baadhi ya nguzo za umeme zilizolazwa chini katika baadhi ya vijiji vya Wilaya ya Chemba.*

nguzo kulazwa chini kwa muda mrefu, zikifika ndani ya siku tatu zisimikwe na zijengwe ili wananchi wapate umeme.”

Akizungumzia uwashaji wa umeme katika kijiji cha Farkwa, Dkt. Kalemani alisema tukio hilo linafanya idadi ya vijiji vya Wilaya ya Chemba vilivyofikiwa nishati ya umeme kufikia 85 kati ya vijiji 114, na kuwaahidi wananchi wa eneo hilo kuwa vijiji vyote vilivyosalia pia vitafikiwa na umeme ndani ya muda uliopangwa.

Aidha, Dkt. Kalemani aliwaagiza Mameneja wa REA na TANESCO kuhakikisha vijiji vilivyobaki katika kata ya Farkwa vinafikishiwa nishati hiyo ndani ya miezi miwili ijayo na kumuelekeza Mkuu wa Wilaya ya Chemba, Saimon Odunga kusimamia suala hilo.

Pia, alitumia fursa hiyo kuwahimiza wananchi kutumia umeme kwa kuanzisha shughuli za kiuchumi ikiwamo uanzishwaji wa viwanda vidogo vidogo na kusema hiyo itawezesha kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja.

“Haiwezekani serikali ikatoa fedha ya kuwafikishia wananchi umeme tena kwa gharama nafuu, halafu wewe mwananchi usiutumie, tutapita kila kaya kukagua na tukikuta hujaweka umeme tutapiga mnada na kuuza kuku au mbuzi na kukuwekea umeme kwa lazima, hivyo hakikisheni mnajiunganishia nishati hiyo,” alisisitiza.

Pia, aliwasihi wananchi wa Farkwa na maeneo mengine kuhakikisha wanatunza miundombinu ya umeme ili iweze kuwasaidia wananchi.

Naye Mbunge wa Chemba, Juma Nkamia pamoja na kuipongeza serikali kwa kazi ya kuwafikishia wananchi nishati hiyo, aliomba maeneo ambayo bado hayajafikiwa yafikiwe ili wananchi waweze kujiletea maendeleo.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Chemba, Saimon Odunga aliwataka wananchi kuchangamkia fursa ya kuunganishwa umeme kwa shilingi 27,000 kupata huduma hiyo wakati mradi unaendelea.



*Baadhi ya wakazi wa kijiji cha Farkwa wakimsikiliza Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani (hayupo pichani) alipofika katika wilaya hiyo kukagua maendeleo ya usambazaji wa umeme hivi karibuni.*



*Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani (katikati) akizungumza na wakazi wa kijiji cha Babayu wilayani Chemba, baada ya kukagua maendeleo ya usambazaji umeme katika kijiji hicho hivi karibuni.*



*Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya wazee wa kijiji cha Farkwa waliopewa vifaa vya Umeme Tayari (UMETA), baada ya Waziri kuwasha umeme katika kijiji hicho Wilayani Chemba hivi karibuni.*



*Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani (kulia) akipokea zawadi ya mbuzi kutoka kwa mmoja wa wazee wa Kijiji cha Babayu wilayani Chemba, baada ya kukagua maendeleo ya usambazaji umeme katika kijiji hicho hivi karibuni.*

# KAMATI YA BUNGE YAPONGEZA HATUA ZILIZOCHOKULIWA NA SERIKALI KUKAMILISHA MRADI WA KINYEREZI I EXTENSION



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (kulia), akiwaongoza Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, kutembelea Mradi wa Umeme wa Kinyerezi I Extension, Machi 16, 2020. Kulia kwa Waziri ni Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Dunstan Kitandula.*

***Veronica Simba – Dar es Salaam***

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini imeipongeza Serikali kupitia Wizara ya Nishati, kwa hatua ilizochukua katika kuhakikisha Mradi wa umeme wa Kinyerezi I Extension (megawati 185) unakamilika mapema iwezekanavyo.

Mwenyekiti wa Kamati, Dunstan Kitandula alitoa pongezi hizo mbele ya waandishi wa habari, wakati akizungumzia msimamo wa Kamati hiyo baada ya kutembelea Mradi husika uliopo eneo la Kinyerezi jijini Dar es Salaam, Machi 16, 2020.

Alisema, Kamati iliamua kutembelea Mradi huo ili kujiridhisha kuhusu hatua zilizochukuliwa na Serikali baada ya kupata taarifa kwamba Mkandarasi aliyekuwa akitekeleza Mradi husika ambaye ni Kampuni ya Jacobsen Electro AS kutoka Norway, amefilisika hivyo haendelei tena na kazi.

Akieleza zaidi, Kitandula alisema, Kamati ilitaka kujiridhisha kwamba kufilisika kwa Mkandarasi hakuiingizi nchi kwenye migogoro ya kimkataba inayosababisha Taifa kuingia gharama zaidi, lakini pia kujionea hatua zilizochukuliwa katika kuhakikisha Mradi unatekelezwa.

"Kusema kweli sisi kama Kamati tumeridhishwa sana na hatua zilizochukuliwa kuhusiana na suala hili, hivyo kwa niaba ya Kamati nitumie nafasi hii kuipongeza Serikali."

Katika hatua nyingine, Kamati imekiri kuridhishwa na kufurahishwa na uhakika uliotolewa na Serikali kuwa umeme kwa ajili ya matumizi ya Treni ya mwendokasi (SGR) pindi itakapokamilika upo tayari na kwamba hauhusiani na kukamilika au kutokamilika kwa Mradi huo wa upanuzi wa Kinyerezi I.

Kuhusu suala la malipo kwa wakandarasi wa ndani waliokuwa wamepewa mkataba na mwekezaji husika ambaye amefilisika, Kitandula alibainisha kuwa Kamati yake imejiridhisha na maelezo yaliyotolewa na Serikali kuwa mchakato unaohusisha kuainisha mchanganuo wa malipo hayo, uko katika hatua za mwisho ili waanze kulipwa.

Awali, akiwasilisha taarifa fupi ya Mradi kwa Kamati husika, Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani alisema hatua zilizochukuliwa na Serikali katika kuhakikisha nchi haipati hasara baada ya Mkandarasi kufilisika ni pamoja na kuhakikisha vifaa vyote vinavyohusika katika utekelezaji wa mradi viko katika eneo hilo.

Aidha, alibainisha kuwa Serikali ilijiridhisha kuwa malipo yaliyofanyika kwa Mkandarasi huyo ni yale tu yanayoendana na kiwango cha kazi aliyofanya na siyo zaidi.

"Mkandarasi amekamilisha kazi kwa wastani wa takribani asilimia 85 na amelipwa kwa kazi ya asilimia 68 hivyo hakuna hasara," alifafanua Waziri.

Aliongeza kuwa, Serikali kwa kushirikiana na taasisi nyingine mbalimbali ikiwemo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, imejipanga kuhakikisha kazi iliyobaki, ambayo ni takribani asilimia 14, inakamilika ndani ya kipindi kisichozidi mwezi Desemba mwaka huu.

"Nimeshatoa maelekezo kwa wataalamu kutoka taasisi zote zinazohusika kuhakikisha tunampata Mkandarasi mwingine ndani ya siku 30 zijazo ili aanze kazi mara moja na kukamilisha kabla ya Desemba."

Akieleza zaidi, Dkt Kalemani alisema Serikali imedhamiria kumpata Mkandarasi mwenye uwezo ambaye gharama yake haitazidi mpango mahsusi wa gharama halisi ya mradi.

Naye Meneja wa Mradi huo, Mhandisi Abdallah Chikoyo, aliwaeleza Wajumbe wa Kamati kuwa, jumla ya miradi saba ya umeme unaotokana na gesi imepangwa kutekelezwa na Serikali.

Aliitaja miradi hiyo kuwa ni pamoja na wa Kinyerezi I (megawati 150) ambao ulikamilika mwaka 2016, Kinyerezi I Extension (megawati 185) ambao ndiyo uliotembelewa na Kamati na uko katika hatua za mwisho kukamilika pamoja na Kinyerezi II (megawati 148) uliokamilika mwaka 1918.

Mwingine ni Mradi wa Kinyerezi III utakaotekelezwa kwa awamu mbili huku kila awamu ikitarajiwa kuzalisha megawati 300. Utekelezaji wake uko katika hatua za kukamilisha utafiti na upembuzi yakinifu ili uanze kutekelezwa.

Mhandisi Chikoyo alitaja miradi mingine kuwa ni Kinyerezi IV (megawati 430), Mradi wa Mtwara (megawati 300) pamoja na Mradi wa Somanga Fungu (megawati 350 hadi 370).

Mradi wa Kinyerezi I Extension unagharamiwa na Serikali ya Tanzania kwa asilimia 100 na gharama yake ni Dola za Marekani milioni 188 sawa na shilingi za Tanzania takribani 435.48.



*Meneja wa Mradi wa Umeme wa Kinyerezi I Extension, Mhandisi Abdallah Chikoyo (kulia), akitoa maelezo kuhusu Mradi huo kwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, walipotembelea eneo hilo, Machi 16, 2020. Wa tatu kutoka kulia ni Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani na kulia kwake ni Mwenyekiti wa Kamati husika, Dunstan Kitandula.*

# MATUKIO PICHANI





Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Dunstan Kitandula (mbele) na Wajumbe wa Kamati hiyo, wakikagua Mradi wa Umeme wa Kinyerezi I Extension, Machi 16, 2020.



Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani akiwasilisha maelezo mafupi ya utekelezaji wa Mradi wa Umeme wa Kinyerezi I Extension kwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, baada ya kutembelea Mradi huo Machi 16, 2020 jijini Dar es Salaam.



Sehemu ya mitambo iliyopo katika Mradi wa Umeme wa Kinyerezi I Extension jijini Dar es Salaam. Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini (hawapo pichani), walitembelea Mradi huo, Machi 16 mwaka huu.











Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, wakikagua Mradi wa Umeme wa Kinyerezi I Extension uliopo jijini Dar es Salaam, Machi 16, 2020.

# WAKANDARASI MRADI WA UMEME PERI-URBAN WATAKIWA KUMALIZA KAZI MWEZI JUNI



*Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (kushoto) na Naibu Waziri wa Nishati Subira Mgalu (kulia) wakiwa kwenye kikao na Wakandarasi wanaotekeleza Mradi wa Umeme wa Peri Urban (hawapo pichani), jijini Dodoma, Machi 19, 2020.*

**Hafsa Omar - Dodoma**

Wakandarasi wanaotekeleza mradi wa umeme pembezoni mwa miji (Peri-Urban) wametakiwa kukamilisha kazi ya usambazaji umeme katika maeneo waliyopangiwa ifikapo Juni mwaka huu (2020) la sivyo watachukuliwa hatua za kisheria.

Maagizo hayo yametolewa na Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani, Machi 19, 2020, mkoani Dodoma wakati wa kikao chake na wakandarasi wanaotekeleza mradi huo.

Kikao hicho kilihudhuriwa na Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said, Kaimu Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu Mhandisi Edward Ishengoma, Kamishna Msaidizi wa Umeme, Mhandisi Innocent Luoga pamoja na viongozi wengine mbalimbali wa Wizara na Taasisi.

Dkt Kalemani aliwataka wakandarasi wa mradi huo kuweka mpango madhubuti ambao utabainisha vijiji vyote ambavyo havijawekewa umeme na mpango huo uoneshe ni lini vijiji hivyo vitapelekewa umeme ndani ya muda uliopangwa.

Aidha, aliwataka wakandarasi hao kufanya kazi kwa bidii ili kuhakikisha ndani ya muda waliokubaliana wawe tayari wameanza kuwasha umeme kwenye vijiji, na miezi miwili inayofuata waitumie kusambazia wananchi umeme majumbani.

Aidha, aliwaagiza wakandarasi wote wa mradi huo kupeleka orodha ya vijiji vinavyosambaziwa umeme kwa Wakuu wa Mikoa, Wilaya, Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa ili viongozi hao wasaidie katika ufuatiliaji wa mradi huo.

Pia, aliwataka kuhakikisha kuwa nguzo zote ambazo zimelazwa chini kwenye maeneo yao, ziwe zimesimikwa na nguzo ambazo zimesimikwa bila kuwa na nyaya, zifungwe nyaya ndani ya mwezi huu (Machi).

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu aliwataka wakandarasi hasika kuupa kipaumbele mradi huo muhimu kwa nchi na kwamba kinachotakiwa kwa sasa ni uwashwaji wa umeme katika maeneo hayo.

Alisema, ana imani kuwa, wakandarasi hao watafuata maelekezo aliyoyatoa Waziri wa Nishati na kuyafanyia kazi.

Naye, Katibu Mkuu, Mhandisi Zena Said, aliwakumbusha wakandarasi hao kuwa, Serikali imewapa fursa na kuwaamini hivyo na wao wanatakiwa kutoiangusha kwa kuhakikisha wanakamilisha kazi zao kwa muda uliopangwa.

Vilevile, aliwataka wasimamizi wa miradi hiyo ya umeme kufanya kazi kwa weledi na kuwasimamia ipasavyo wakandarasi hao ili kuhakikisha wanamaliza kazi zao kwa mujibu wa mkataba.



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Zena Said (kushoto) akizungumza jambo wakati wa Mkutano wa Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani (kulia) na Wakandarasi wanaotekeleza Mradi wa Umeme wa Peri Urban (hawapo pichani), jijini Dodoma, Machi 19, 2020.*

# WABUNGE WAUNGA MKONO ZUIO LA SERIKALI UAGIZAJI VIFAA VYA UMEME NJE YA NCHI



*Mmoja wa Wakurugenzi wa Kiwanda cha Europe Inc. Industries Ltd (Tropical), Aloyce Ngowi (kushoto) akiwaonesha Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini vifaa mbalimbali vya umeme vinavyotengenezwa na kampuni hiyo, Machi 14 mwaka huu jijini Dar es Salaam.*



*Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu akizungumza wakati wa majumuisho baada ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kutembelea viwanda vinavyozalisha vifaa mbalimbali vya umeme nchini vya Europe Inc. Industries Ltd (Tropical) na Kilimanjaro Cables (T) Ltd (Africab) vilivyopo jijini Dar es Salaam, Machi 14 mwaka huu.*

**Veronica Simba – Dar es Salaam**

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini imesema inaendelea kuunga mkono zuio la serikali kwa wakandarasi wa miradi mbalimbali ya umeme nchini kuagiza vifaa husika nje ya nchi.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Machi 14 mwaka huu, baada ya Kamati hiyo kufanya ziara katika viwanda vya Europe Inc. Industries Ltd (Tropical) na Kilimanjaro Cables (T) Ltd (Africab), vinavyozalisha nyaya za umeme na mashine umba (transfoma), Mwenyekiti wa Kamati husika, Dunstan Kitandula alisema uamuzi huo ni mzuri na unapaswa kuungwa mkono.

"Baada ya kutembelea viwanda hivi, tumejiridhisha pasipo shaka kuwa uwezo wake wa uzalishaji unatosheleza mahitaji ya ndani hivyo hakuna sababu ya kuagiza vifaa hivyo nje ya nchi," alisema Kitandula.

Akieleza zaidi, Mwenyekiti alisema lengo la ziara yao lilikuwa ni kujiridhisha kuhusu uwezo wa uzalishaji wa viwanda husika kutokana na mkanganyiko uliopo kutokana na baadhi ya wakandarasi kulalamika kuwa vifaa vinavyozalishwa ndani ya nchi havitoshelezi mahitaji yao.

Alisema kumekuwepo na malalamiko kutoka kwa wananchi kuwa kasi ya utekelezaji miradi ya umeme vijijini hairidhishi na wakandarasi husika wanapoulizwa wamekuwa wakijitetea kuwa hali hiyo inasababishwa na zuio la serikali kuagiza vifaa nje ya nchi.

Hata hivyo, Kitandula alisema mara zote Serikali imekuwa ikisisitiza kuwa viwanda vya ndani vina uwezo mkubwa kiuzalishaji kwani unakidhi mahitaji ya soko la ndani na hata kuwepo ziada.

Katika hatua nyingine, Mwenyekiti huyo wa Kamati, alitoa wito kwa Wizara ya Nishati na Wakala wa Nishati Vijijini (REA), kuwasaidia wazalishaji wa ndani katika utafutaji masoko ya vifaa husika ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na katika Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC).

"Ni lazima sasa ninyi Wizara na REA mvichukulie viwanda hivi kama sifa kwa nchi na mvisaidie kupata masoko nje ya nchi ili kuwawezesha wawekezaji hawa wazalendo kuzalisha kwa tija zaidi na kuepuka hasara inayoweza kuwafilisi," alisisitiza.

Akizungumzia hatua zilizochukuliwa na Serikali

ENDELEA UK. 19



*Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Joseph Kasheku Musukuma, akizungumza na baadhi ya waajiriwa wa Kampuni ya kuzalisha vifaa vya umeme ya Europe Inc. Industries Ltd (Tropical) kuhusu kazi wanayoifanya, wakati Kamati husika ilipotembelea kiwanda hicho Machi 14 mwaka huu jijini Dar es Salaam.*

# WABUNGE WAUNGA MKONO ZUIO LA SERIKALI UAGIZAJI VIFAA VYA UMEME NJE YA NCHI



*Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Ally Kessy, akizungumza na baadhi ya waajiriwa wa Kampuni ya kuzalisha vifaa vya umeme ya Europe Inc. Industries Ltd (Tropical) kuhusu kazi wanayoifanya, wakati Kamati husika ilipotembelea kiwanda hicho Machi 14 mwaka huu jijini Dar es Salaam.*



*Kaimu Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Mhandisi Edward Ishengoma (wa pili-kushoto) akijadiliana jambo na mmoja wa Wakurugenzi wa Kiwanda cha Europe Inc. Industries Ltd (Tropical), Aloyce Ngowi kuhusu vifaa mbalimbali vya umeme vinavyozalishwa kiwandani hapo, wakati Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ilipotembelea kiwanda hicho Machi 14 mwaka huu jijini Dar es Salaam.*

katika suala hilo, Naibu Waziri wa Nishati Subira Mgalu, alisema Wizara imeendelea kuwasaidia wawekezaji wa ndani katika utafutaji masoko nje ya nchi akitoa mfano namna serikali ilivyoisaidia kampuni ya Africab ilipotaka kuwekeza nchini Zambia.

"Niwapongeze Africab kwa uthubutu wao ambao umewawezesha kuanzisha kiwanda nchini Zambia. Walipoenda huko mara ya kwanza, tuliwasaidia kuzungumza na Serikali ya nchi hiyo tukawaeleza uwezo wao wa ndani hatua iliyowasaidia kufanikisha lengo lao. Tutaendelea kufanya hivyo kwa kampuni zetu nyingine," alisema Naibu Waziri.

Kuhusu suala la baadhi ya wakandarasi wanaosemekana kuendelea kuagiza vifaa nje ya nchi, Naibu Waziri alisisitiza kuwa msimamo wa Serikali ni kutoa adhabu kali za kimkataba na kisheria kwa yeyote atakayebainika kama alivyobainisha Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani hivi karibuni.

Kiwanda cha Africab kina uwezo wa kuzalisha (kwa mwaka) nyaya za umeme kilomita 75,000 transfoma 6,500 na insulators 660,000 wakati Kiwanda cha Tropical kikiwa na uwezo wa kuzalisha transfoma 75,000 na nyaya zinazozidi kwa kiasi kikubwa mahitaji ya soko la ndani.

Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini iko katika ziara jijini Dar es Salaam na Mkoa wa Pwani, kukagua miradi mbalimbali inayotekelezwa chini ya Wizara ya Nishati.

# Dkt kalemani aagiza Msimamizi Mkuu wa SCADER achukuliwe hatua

*Zuena Msuya - Mtera*

Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani amemuagiza Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Dkt. Tito Mwinuka kumchukulia hatua Msimamizi Mkuu wa mfumo wa kusafirisha umeme kwa njia ya kieletroniki katika Gridi ya Taifa (SCADER), Abubakar Issa ambaye amekaidi agizo la Waziri lililomtaka kuishi ndani ya kituo cha kupoza na kusambaza umeme cha Ubungo.

Dkt. Kalemani alitoa agizo hilo Machi 20, 2020, baada ya kufanya ziara ya kutembelea mabwawa ya kufua na kuzalisha umeme wa maji ya Kidatu na Mtera kwa lengo la kuona hali ya usalama, uzalishaji wa umeme katika mitambo hiyo, kiwango cha maji katika mabwawa pamoja na baadhi ya miundombinu ya kusafirisha umeme iliyopata hitilafu kufuatia mvua kubwa zinazoendelea kunyesha.

Akielezea maagizo aliyotoa awali, alisema kuwa alimtaka Mkuu huyo wa SCADER, Abubakar Issa kuhamia katika nyumba za serikali zilizopo ndani ya eneo la kituo cha kupoza na kusambaza umeme cha Ubungo zilizojengwa mahsusi kwa ajili ya watendaji na wasimamizi wa mfumo huo ili kurahisisha upatikanaji wao pale linapotokea tatizo na kulishughulikia haraka.

"Nilipotembelea Mwezi Novemba, hawa wataalam hawakuwa wakiishi pale, mwezi Desemba niliagiza Issa ahamie lakini hakuhamia, juzi saa tatu na nusu usiku nampigia simu baada ya tatizo kutokea, ananiambia yupo njiani anakwenda katika eneo la tukio kwa maana hiyo hajahamia pale bado, ndiyo maana nimeagiza achukuliwe hatua. Mkurugenzi usipochukua hatua wewe, mimi nitachukua. Sasa nachukua hatua gani na kwa nani itajulikana hapo," alisisitiza Dkt. Kalemani.

Alisema kuwa alishaagiza watendaji na watumishi wote wanaotakiwa kukaa na kuishi kwenye vituo vya kufua na kuzalisha umeme (Plant) pamoja na vituo vya kupoza na kusambaza umeme (Substation) wakae humo ili kama tatizo linatokea warekebishe mara moja lakini imekuwa ikichukua saa mbili hadi tatu kurekebisha hitilafu.

Akieleza Zaidi, Dkt. Kalemani alisema kuwa alipokea simu kutoka mkoani Mwanza, wananchi wakilalamika juu ya kukatiwa umeme kwa saa mbili, alipohoji alielezwa kuwa Abubakar ndiye aliyeagiza umeme huo ukwate bila sababu maalumu.

"Sitakubali kufanya kazi na watendaji wanaocheza na maisha ya watu kwa kutowajibika, bora nibaki na watu wachache wenye uzalendo na weledi wa kuwatumikia wananchi na Tanzania kwa ujumla kuliko kuwa na wengi wasio na tija kwa maslahi ya taifa," alisisita Dkt. Kalemani.

Kwa mara ya kwanza Dkt. Kalemani alitoa agizo la kuwataka wataalamu hao kuhamia katika nyumba hizo Oktoba 3, 2019, Jijini Dar es Salaam, baada ya kutembelea kituo hicho ili kubaini chanzo cha hitilafu ya umeme iliyotokea katika Kituo cha Kupoza na Kusambaza umeme cha Ubungo na kusababisha Mkoa huo pamoja na Zanzibar kukosa umeme kwa muda wa saa kadhaa usiku wa kuamkia tarehe hiyo.

Katika maagizo yake, Dkt. Kalemani, aliagiza kusimamishwa kazi kwa uzembe, Msimamizi aliyekuwepo zamu siku hiyo kwa kushindwa kubaini chanzo cha hitilifu. Pia aliagiza watumishi sita akiwemo Msimamizi Mkuu wa SCADER kuhamia katika nyumba hizo siku hiyo ya Oktoba 3 mwaka jana, hadi kufikia saa nane mchana wa siku hiyo.

# SERIKALI YAPONGEZWA KUUNGANISHA GESI ASILIA VIWANDANI

***Veronica Simba – Dar es Salaam***

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini imeipongeza serikali kuunganisha gesi asilia katika viwanda mbalimbali nchini jambo ambalo limesaidia kupunguza gharama za uendeshaji.

Kaimu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Vedastus Mathayo, alitoa pongezi hizo, Machi 17, 2020 baada ya Wajumbe wa Kamati kutembelea Kiwanda cha kufua vyuma cha Lodhia, kilichopo

ENDELEA UK. 21



*Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, wakimsikiliza Meneja Mkuu wa Kiwanda cha kufua vyuma cha Lodhia, kilichopo Mkuranga, Raju Singh (kushoto), walipotembelea kiwanda hicho Mach 17, 2020 kujionea namna kinavyonufaika na matumizi ya gesi asilia. Wa pili kutoka kushoto ni Kaimu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Vedastus Mathayo na katikati ni Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu.*

# SERIKALI YAPONGEZWA KUUNGANISHA GESI ASILIA VIWANDANI

Mkuranga mkoani Pwani kwa lengo la kujionea manufaa yaliyopatikana kutokana na matumizi ya gesi asilia.

"Kama Kamati, tumefurahishwa sana na mafanikio yaliyopatikana baada ya kiwanda hiki kuunganishiwa mtandao wa gesi asilia na tunaipongeza sana Serikali kupitia Wizara ya Nishati," amesema Mathayo.

Pamoja na pongezi hizo, Kamati imeishauri serikali kuendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kuzalisha umeme ambayo itasaidia upatikanaji wa nishati hiyo kwa wingi hivyo kuwezesha gharama yake kupungua na hivyo kuwawezesha wawekezaji katika viwanda kuzalisha kwa tija zaidi.

Akitoa maelezo ya serikali kutokana na maelekezo hayo yaliyotolewa na Kamati, Naibu Waziri wa Nishati Subira Mgalu, ambaye alimwakilisha Waziri mwenye dhamana, Dkt Medard Kalemani, alisema Serikali itahakikisha inaendelea kusimamia kikamilifu miradi mbalimbali ya uzalishaji umeme ili kuwezesha upatikanaji wa umeme mwingi na wa uhakika wenye gharama nafuu.

"Tuna matumaini kwamba kukamilika kwa miradi mikubwa, ukiwemo wa Julius Nyerere (MW 2,115) kutawezesha kushuka gharama za umeme kwa kiasi kikubwa."

Awali, akiwasilisha taarifa ya kiwanda hicho mbele ya Wajumbe wa Kamati, Meneja Rasilimaliwatu, Martin Mkange alisema kupatikana kwa gesi asilia kumewasaidia pamoja na mambo mengine kuondokana na matumizi ya mafuta mazito ambayo yalikuwa na gharama kubwa katika uendeshaji.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kwa Kamati, Kiwanda cha Lodhia kinatumia gesi asilia kiasi cha wastani wa futi za ujazo milioni 0.1 hadi 0.2 kwa siku, sawa na makusanyo ya zaidi ya shilingi milioni 70 kwa mwezi.

Taarifa inaeleza zaidi kuwa kiwanda hicho kilianza kutumia gesi asilia mwezi Juni, 2019.

Miradi ya usambazaji gesi asilia nchini inaendelea kutekelezwa katika maeneo ambayo tayari kuna miundombinu wezeshi ikihusisha mikoa ya awali ya Pwani na Dar es Salaam.



*Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu (katikati), akiwaongoza Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, kukagua kiwanda cha kufua vyuma cha Lodhia, kilichopo Mkuranga mkoani Pwani, Machi 17, 2020. Ziara ya Kamati ililenga kujionea matumizi ya gesi asilia kiwandani hapo.*



*Kazi ya kufua vyuma ikiendelea katika kiwanda cha Lodhia kilichopo Mkuranga, mkoani Pwani. Taswira hii ilichukuliwa wakati wa ziara ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini (hawapo pichani) kiwandani hapo, Machi 17 mwaka huu, kwa lengo la kujionea matumizi ya gesi asilia.*



*Sehemu ya shehena ya vyuma ambavyo vimetengenezwa na kiwanda cha Lodhia kilichopo Mkuranga mkoani Pwani. Taswira hii ilichukuliwa wakati wa ziara ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini (hawapo pichani) kiwandani hapo, Machi 17 mwaka huu, kwa lengo la kujionea matumizi ya gesi asilia.*







*Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini wakiwa katika ziara iliyolenga kujionea matumizi ya gesi asilia katika kiwanda cha kufua vyuma cha Lodhia kilichopo Mkuranga mkoani Pwani, Machi 17 mwaka huu.*

# WAZIRI AKERWA NGUZO ZA UMEME KUTOSIMIKWA



Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (mwenye miwani-kulia), akimwagiza Mkandarasi kutoka Kampuni ya Namis Corporate Ltd), anayetekeleza mradi wa Umeme wa Peri-Urban katika Mtaa wa Viwege, Kata ya Majohe, wilayani Ilala, mkoani Dar es Salaam, kuziondoa nguzo zilizorundikwa chini na kuzisimika mara moja kisha awaunganishie wananchi husika umeme. Alitoa maagizo hayo Machi 12 mwaka huu akiwa katika ziara ya kazi.



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (katikati), akimwagiza Mkandarasi kutoka Kampuni ya Namis Corporate Ltd), anayetekeleza mradi wa Umeme wa Peri-Urban katika Mtaa wa Bombambili, wilayani Ilala, mkoani Dar es Salaam, kuhakikisha anawaunganishia umeme wananchi wote waliolipia ifikapo mwisho wa mwezi huu (Machi, 2020). Alitoa maagizo hayo Machi 12 mwaka huu, akiwa katika ziara ya kazi.*

**Veronica Simba – Dar es Salaam**

Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani ameonesha kukerwa na tabia ya wakandarasi wanaorundika nguzo za umeme katika maeneo mbalimbali kwa muda mrefu pasipo kuzisimika ili kuwaunganishia umeme wananchi.

Hali hiyo ilidhihirika Machi 12 mwaka huu aliposhuhudia rundo la nguzo zikiwa chini katika mtaa wa Viwege, Kata ya Majohe, wilayani Ilala, Mkoa wa Dar es Salaam, akiwa katika ziara ya kazi.

Kufuatia hali hiyo, Dkt Kalemani alimwagiza Mkandarasi anayetekeleza mradi wa umeme pembezoni mwa miji (Peri-Urban) katika eneo hilo (kampuni ya Namis Corporate Ltd) kuziondoa nguzo hizo mara moja na kuzisimika kisha kuwaunganishia umeme wananchi husika.

"Asipotekeleza agizo langu kufikia kesho asubuhi, nawaomba Diwani na Mwenyekiti wa Mtaa mnipigie simu na kunijulisha ili nimchukulie hatua mara moja," alisisitiza Waziri.

Aidha, alisema agizo hilo liwafikie wakandarasi wote wanaotekeleza miradi mbalimbali ya umeme nchini kote kwamba hawatakiwi kurundika nguzo chini pasipo sababu ya msingi, wakati wananchi wakiendelea kulalamika kutounganishiwa huduma hiyo kwa wakati.

Sambamba na agizo hilo, Waziri pia alimwagiza Mkandarasi huyo kuhakikisha anawaunganishia umeme wananchi wote waliolipia huduma hiyo katika maeneo anakotekeleza mradi yakihusisha Kivule Bombambili, Viwege, Majohe na Dondwe kabla ya mwisho wa mwezi huu wa Machi, 2020 vinginevyo hatua kali za kimkataba zitachukuliwa dhidi yake.

"Nawaahidi mimi mwenyewe nitarudi hapa ifikapo mwisho wa mwezi ili kujiridhisha endapo maagizo yangu yametekelezwa. Ikitokea nikashindwa kuja mimi, nitamtuma mwakilishi aje kukagua na kuniletea mrejesho."

Akiwa katika ziara hiyo ya siku moja, Waziri alikataa kuwasha umeme katika Mtaa wa Bombambili kutokana na idadi ndogo ya wateja waliounganishwa na kueleza kuwa atarudi kufanya kazi hiyo baada ya mkandarasi kutekeleza maagizo yake ya kuwaunganishia umeme wateja wote watakaokuwa wamelipia ndani ya kipindi cha mwezi mmoja.

Kufuatia utekelezaji duni wa mradi husika katika maeneo hayo, Waziri aliagiza Fundi Mchundo kutoka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), anayesimamia mradi huo katika maeneo husika, kuondolewa katika nafasi hiyo na ateuliwe mwingine mara moja.

Akizungumza kwa niaba ya wananchi, Diwani wa Kata ya Tengerea, Shabani Manda, alimshukuru Waziri kwa kufanya ziara hiyo pamoja na maagizo aliyoyatoa akisema anaamini wananchi wa maeneo hayo watanufaika na huduma hiyo ya umeme kwa kuanzisha biashara mbalimbali zitakazowasaidia kuwainua kiuchumi.

Katika ziara hiyo, Waziri alifuatana na viongozi na wataalamu mbalimbali kutoka wizarani, TANESCO na Wakala wa Nishati Vijijini (REA), akiwemo Kamishna Msaidizi wa Umeme, Mhandisi Innocent Luoga.



*Mafundi wakifunga Mashine Umba (Transfoma) katika eneo la Dondwe, wilayani Mkuranga, Mkoa wa Pwani, wakati Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani na Ujumbe wake, walipotembelea eneo hilo kujionea maendeleo ya kazi husika, Machi 12 mwaka huu.*

# MATUKIO *PICHANI*



Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (wa pili-kulia), akitoa maelekezo mbalimbali kwa Mkandarasi kutoka Kampuni ya Namis Corporate Ltd), anayetekeleza mradi wa Umeme wa Peri-Urban katika Mtaa wa Viwege, Kata ya Majohe, wilayani Ilala, mkoani Dar es Salaam, kufunga nyaya za umeme katika nguzo alizosimika na kuwaunganishia nishati hiyo wananchi wa eneo hilo. Waziri alitoa maagizo hayo Machi 12 mwaka huu, akiwa katika ziara ya kazi.



Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (mwenye miwani-mbele), akikagua utekelezaji wa Mradi wa Umeme wa Peri-Urban katika Mtaa wa Bombambili, wilayani Ilala, Mkoa wa Dar es Salaam, akiwa katika ziara ya kazi, Machi 12 mwaka huu.







Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini wakiwa katika ziara iliyolenga kujionea matumizi ya gesi asilia katika kiwanda cha kufua vyuma cha Lodhia kilichopo Mkuranga mkoani Pwani, Machi 17 mwaka huu.

# Dkt. Kalemani asema Corona isiwe kisingizio cha kutokamilisha miradi ya umeme




*Jiwe la msingi lililowekwa na Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani ikiwa ni kuzindua na kuwasha taa zinazotumia mwanga wa jua (Solar) katika mitaa ya Wilaya ya Chato Mkoani Geita hivi karibuni.*




*Mwonekano wa Kituo kipya cha Afya cha Bwina nyakati za usiku baada ya Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani kuwasha umeme katika kituo hicho hivi karibuni.*

***Zuena Msuya - Geita***

Waziri wa Nishati, Dkt Medard Kalemani amewataka wakandarasi wanaotekeleza miradi ya usambazaji wa umeme vijijini, kujikinga na kuchukua tahadhari dhidi ya virusi vya Corona (COVID-19) ili waweze kuendelea kutekeleza miradi hiyo na kuikamilisha kwa wakati unaotakiwa kwa mujibu wa mikataba.

Dkt Kalemani alisema hayo Machi 26, 2020, wakati akiwasha umeme katika Kituo cha Afya Bwina, kuwasha taa za barabarani zinazotumia mwanga wa jua (Solar) ambapo pia aliwahamasisha wananchi wa Wilaya ya Chato kuendelea kuchukua tahadhari na kujikinga dhidi ya virusi vya Corona.

Akifafanua, alisema kuwa tishio dhidi ya kuwepo kwa virusi vya Corona kusirudishe nyuma juhudi za utekelezaji wa miradi ya usambazaji umeme vijijini kwa kuwa tayari Mamlaka husika zimetoa miongozo ya kujikinga na kujihadhari dhidi ya virusi hivyo katika maeneo mbalimbali nchini.

"Tujikinge na tuchukue tahadhari dhidi ya Corona lakini kazi ya kusambaza umeme vijijini lazima iendelee, tena kwa kasi ya hali ya juu na miradi ikamilishwe kwa wakati uliopangwa."

Akieleza zaidi alisema jambo la muhimu ni kwa wakandarasi kufuata miongozo iliyotolewa na Mamlaka husika ili waweze kutekeleza majukumu yao.

Waziri aliendelea kuwasisitiza wakandarasi kutotumia kisingizio cha kuwepo virusi vya Corona kuchelewesha ama kutokamilisha miradi ya kusambaza umeme vijijini pamoja na ujenzi wa mradi mkubwa wa kufua umeme kwa kutumia maji wa Mwalimu Nyerere.

Alisema Mamlaka husika zimeweka wazi na kuendelea kutoa matangazo kila kona ya nchi kuhusu namna bora ya kujikinga na kuchukua tahadhari dhidi ya virusi vya Corona, hivyo wakandarasi katika maeneo yao ya kazi wanapaswa kuhakikisha wanasimamia na kutekeleza miongozo hayo.

Akizindua na kuwasha taa za barabarani katika mitaa ya Wilaya ya Chato mkoani Geita, Dkt Kalemani alisema kuwa lengo la kuweka taa hizo ni kuongeza usalama kwa wananchi wanaotumia barabara hizo nyakati za usiku.


Aidha, Dkt Kalemani aliwasha umeme katika Kituo kipya cha afya cha Bwina wilayani humo ili kurahisisha upatikanaji wa huduma za afya wakati wote kwa wagonjwa wanaofika kutibiwa katika kituo hicho.

Aliwataka wananchi kulinda miundombinu ya taa hizo pamoja na kuitunza ili idumu kwa muda mrefu kwa faida yao na kuwahimiza kwenda kutibiwa wakati wote katika kituo cha afya cha Bwina.

Katika ziara hiyo, vilevile aliwasisitiza wananchi kuendelea kutekeleza maagizo na maelekezo yanayoendelea kutolewa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na wadau mbalimbali wa afya ya kujikinga dhidi ya Virusi vya Corona, ikiwemo kunawa mikono mara kwa mara, kuepuka misongamano na mikusanyiko na kutoa taarifa pale tu wanapomuona mtu mwenye dalili za ugonjwa huo kama zinavyoelezwa katika matangazo.

Dkt. Kalemani alikuwa akifanya ziara yake hiyo pasipo kuwa na mikutano ya kuzungumza na wananchi, kusimama umbali mrefu kati yake na baadhi ya watu alioambatana nao pamoja na vyombo vya habari na kunawa mikono na kupaka kitakasa mikono kila akifika eneo husika ili kujikinga dhidi ya virusi vya Corona.

Ikumbukwe kuwa Machi 24, 2020, katika Mkutano wa Baraza la Mawaziri, Waziri Mkuu, Kasim Majaliwa alielekeza kuwa sehemu kubwa ya ziara ya Mawaziri katika kutekeleza majukumu yao, iwe ni kuwahamasisha wananchi kuendelea kuchukua tahadhari na kujinga dhidi ya virusi vya Corona, kwa kufuata njia bora na sahihi zinazotolewa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.



*Muonekano wa barabara za Mitaa ya Chato nyakati za usiku baada ya Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani kuzindua na kuwasha taa zinazotumia mwanga wa Jua (Solar) hivi karibuni.*

# WAZIRI KALEMANI ATOA NENO UAGIZWAJI VIFAA VYA UMEME NJE YA NCHI

*Veronica Simba – Dar es Salaam*

Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani amesisitiza msimamo wa serikali kutoruhusu uagizwaji nje ya nchi, vifaa vya umeme hususan mashine umba (transfoma) na nyaya na kwamba atakayebainika kukaidi agizo hilo atachukuliwa hatua kali za kisheria zinazohusiana na uhujumu uchumi.

Alitoa msimamo huo jijini Dar es Salaam, Machi 12 mwaka huu, baada ya kutembelea kiwanda cha Europe Inc. Industries LTD (TROPICAL), kinachozalisha vifaa hivyo na kujiridhisha kuwa uwezo wake unatosheleza mahitaji ya sasa nchini.

Akiwa ameambatana na Kamishna Msaidizi wa Umeme, Mhandisi Innocent Luoga pamoja na wataalamu mbalimbali kutoka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Waziri alitoa tamko rasmi la serikali kuwa msimamo wake unabaki palepale.

Alisema, miradi mingi ya umeme imekuwa ikichelewa huku wakandarasi husika wakilalamika kuwa wanakwamishwa na ukosefu wa vifaa, jambo ambalo serikali imejiridhisha kuwa siyo kweli.

Akitoa mfano wa uwezo wa uzalishaji kwa kiwanda hicho alichotembelea, Dkt Kalemani alibainisha kuwa kinazalisha zaidi ya mashine umba 75,000 kwa mwaka wakati mahitaji ya nchi ni 21,000 pekee.

"Sasa, hawa tu peke yake wanazalisha zaidi ya mahitaji yetu ukiachilia mbali viwanda vingine tulivyonavyo nchini ambavyo ni pamoja na TANALEC, AFRI-CABLE na wengineo," alibainisha.

Aidha, aliongeza kuwa, kwa upande wa nyaya, baadhi ya wakandarasi wamekuwa wakilalamika kwamba hazitoshelezi mahitaji jambo ambalo alisema siyo kweli kwani baada ya kukagua amejiridhisha kuwa kiwanda hicho pekee kina shehena ya kutosha.

Kuhusu malalamiko ya uhaba wa mashine umba za KVA 11, Waziri alibainisha kuwa amejiridhisha zipo nyingi zinazotosheleza mahitaji na alitoa maagizo kwa watendaji wa REA kuanza mara moja kuchukua oda yao waliyokuwa wameagiza kiwandani hapo ili miradi ya umeme vijijini iendelee kutekelezwa kwa kasi kutokana na uhitaji walionao wananchi kwa nishati hiyo muhimu.



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (katikati), akisikiliza maelezo kuhusu kiwanda cha kuzalisha nyaya za umeme na mashine umba (transfoma) kinachomilikiwa na kampuni ya Europe Inc. Industries LTD (TROPICAL) kutoka kwa Meneja Mkuu, Pamela Irengo (kulia kwa Waziri), alipotembelea kiwanda hicho Machi 12 mwaka huu jijini Dar es Salaam. Kushoto kwa Waziri ni Kamishna Msaidizi wa Umeme, Mhandisi Innocent Luoga.*

Katika hatua nyingine, Waziri aliwapongeza wamiliki wa kiwanda hicho ambao pia kampuni yao (State Grid Electrical & Technical Works Ltd) ni moja ya zilizopewa dhamana na serikali kutekeleza miradi ya umeme vijijini, huku akiwaasa wakandarasi wengine nchini kuiga mfano wao kwa kuanzisha viwanda vyao wenyewe vyenye kuzalisha vifaa watakavyotumia katika kutekeleza miradi hiyo pamoja na kuwauzia wengine.

Hata hivyo, aliiagiza kampuni hiyo kuhakikisha inakamilisha kazi yake katika mikoa iliyopewa kimkataba ya Lindi na Morogoro kufikia mwezi ujao (Aprili) kwani hakuna sababu ya kutotekeleza kwa wakati ilhali vifaa wanavyo.

Awali, wakizungumza kwa nyakati tofauti wakati wakitoa salamu za ukaribisho kwa Waziri, wamiliki wa kiwanda, Aloyce Ngowi na Charles Mlawa pamoja na Meneja Mkuu Pamela Irengo, waliishukuru Serikali ya Awamu ya Tano, wakisema ndiyo iliyowatia chachu ya kuanzisha kiwanda hicho.

"Tulipata hamasa kutoka kwa Rais John Magufuli kutokana na msisitizo wake katika kujenga uchumi wa viwanda, hivyo nasi tukaitumia fursa hii ipasavyo."

Aidha, walimpongeza Waziri Kalemani na watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiwapatia katika utendaji kazi wao.

Kampuni hiyo inayomilikiwa na wazawa kwa asilimia 100 imeajiri wafanyakazi 300 ambao wote ni watanzania na imeanza mchakato wa kupanua kiwanda husika kitakachojengwa eneo la Kisemvule wilayani Temeke ili kukidhi kwa ufanisi zaidi mahitaji ya wateja wake.



*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (mwenye miwani-katikati), akisikiliza maelezo kuhusu uzalishaji nyaya za umeme kutoka kwa mmoja wa wakurugenzi wa kampuni ya Europe Inc. Industries LTD (TROPICAL), Charles Mlawa, alipotembelea kiwanda hicho kinachozalisha mashine umba (transfoma) na nyaya za umeme, Machi 12, 2020.*

# WAZIRI KALEMANI ATOA NENO UAGIZWAJI VIFAA VYA UMEME NJE YA NCHI



*Mmoja wa waajiriwa wa kiwanda cha kutengeneza mashine umba (transfoma) na nyaya za umeme, kinachomilikiwa na kampuni ya Europe Inc. Industries LTD (TROPICAL), Farida Karim akiwa kazini. Taswira hii ilichukuliwa wakati wa ziara ya Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (hayupo pichani) kiwandani hapo, eneo la Mwenge jijini Dar es Salaam, Machi 12 mwaka huu.*





*Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani na Ujumbe wake, wakikagua sehemu mbalimbali za kiwanda cha kuzalisha nyaya za umeme na mashine umba (transfoma) kinachomilikiwa na kampuni ya Europe Inc. Industries LTD (TROPICAL) iliyopo Mwenge jijini Dar es Salaam, akiwa katika ziara ya kazi, Machi 12 mwaka huu.*



*Sehemu ya shehena ya mashine umba (transfoma) zinazozalishwa na kampuni ya Europe Inc. Industries LTD (TROPICAL) iliyopo Mwenge jijini Dar es Salaam. Taswira hii ilichukuliwa wakati wa ziara ya Waziri wa Nishati Dkt Medard Kalemani (hayupo pichani) kiwandani hapo, Machi 12 mwaka huu.*

## MATUKIO *PICHANI*

# MATUKIO MBALIMBALI WAKATI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI ILIPOFANYA ZIARA KATIKA MRADI WA UMEME WA KINYEREZI I EXTENSION JIJINI DAR ES SALAAM, MACHI 16, 2020













# MATUKIO MBALIMBALI WAKATI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI ILIPOFANYA ZIARA KATIKA MRADI WA UMEME WA KINYEREZI I EXTENSION JIJINI DAR ES SALAAM, MACHI 16, 2020











# MATUKIO MBALIMBALI WAKATI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI ILIPOTEMBELEA KIWANDA CHA KUZALISHA VIFAA VYA UMEME CHA KILIMANJARO CABLES (AFRICAB), KILICHOPO JIJINI DAR ES SALAAM, MACHI 14, 2020













# MATUKIO MBALIMBALI WAKATI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI ILIPOTEMBELEA KIWANDA CHA KUZALISHA VIFAA VYA UMEME CHA KILIMANJARO CABLES (AFRICAB), KILICHOPO JIJINI DAR ES SALAAM, MACHI 14, 2020









# MATUKIO *PICHANI*

## MATUKIO MBALIMBALI WAKATI WAJUMBE WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI WALIPOTEMBELEA KIWANDA CHA KUTENGENEZA VIFAA VYA UMEME CHA EUROPE INC. INDUSTRIES LTD (TROPICAL) KILICHOPO MWENGE JIJINI DAR ES SALAAM, MACHI 14, 2020













# MATUKIO MBALIMBALI WAKATI WAJUMBE WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI WALIPOTEMBELEA KIWANDA CHA KUTENGENEZA VIFAA VYA UMEME CHA EUROPE INC. INDUSTRIES LTD (TROPICAL) KILICHOPO MWENGE JIJINI DAR ES SALAAM, MACHI 14, 2020

